(Mwezesaji ataandika sentensi ifuatayo na kujadiliwa na timu ya kuandaa mpango na sheria ndogo.)

Mwangalizi mkuu wa msitu katika eneo la kijiji cha ni kamati ya msitu ambayo ndio itapanga walenzi wa msitu watakao toka katika vitongoji. Kamati hiyo itafanya kazi zake chini ya kamati ya maliasili (au mazingira?) na itapeleka ripoti zake katika Serikali ya kijiji.

CONTENT OF A BY-LAW FOR VILLAGE FOREST MANAGEMENT AREA

SECTION ONE

INTRODUCTION

(Introduction is written by the facilitator and discussed with the planning team)

This by-law has been made to protect, to develop and to manage sustainably the resources of forest reserve, in the area of village, in Ward, Division, District of Tanga Region.

This by-law has been made in parallel with the management plan of this forest reserve. Both of them consider the objective of protection, the real state of the forest and its environment.

TITLE OF THE BY-LAW

(Title is written by the facilitator and discussed with the planning team)

The name of this by-law is the by-law to manage, protect and conserve the forest reserve in the area of village for sustainable utilization, of year

VOCABULARY OF THIS BY-LAW

(This is written by the facilitator and discussed with the planning team.)

FOREST AREA AND BORDERS

(This chapter is copied from the management plan.)

MAIN SUPERVISOR OF THE FOREST IN THE AREA OF VILLAGE

(The following sentences could be written by the facilitator and discussed with the planning team)

Main supervisor of the forest in the area of village is the forest committee, which will arrange forest guards from the sub-villages. The forest committee works under the natural resources committee (or the environmental committee?) and reports to the village government.

Kamati ya msitu itachaguliwa na mkutano mkuu na itadumu kwa kipindi cha miaka

The forest committee is elected in the village assembly for a period of years.

SEHEMU YA PILI

SECTION TWO

- 6. MATUMIZI YA MAZAO YA MSITU**
(Sura hii imenakiliwa kutoka kwenye mpango.)

UTILIZATION OF FOREST
(This chapter is copied from the management plan.)

- 7. UKAGUZI NA ULINZI WA MSITU**
(Sura hii imenakiliwa kutoka kwenye mpango.)

FOREST PROTECTION
(This chapter is copied from the management plan.)

- 8. ADHABU**
Adhabu gani itolewe kwa wale wanaovuja sheria ndogo hii?
Labda zipo za kimila/kijadi je mnapenda ziendeleo, zibadishwe kuwa kiwango chapesa?
Namna gani mhalifu ashughuliwe au makosa yashughuliwe vipi?
Kiasi gani cha faini au fidia kitumike? Endapo mhalifu ni mwanakamati au kiongozi wa serikali ya kijiji au mjumbe wa serikali ya kijiji aadhibiwe kwa faini mara mbili au?
Adhabu zingine? Kwa mfano, mhalifu apewe kazi maalumu za msaragambo. Mhalifu kama akikataa adhabu afanyweje?

PENALTIES
What type of penalties should be imposed to the offenders?
Maybe there are traditional or customary penalties which could be used?
How the offender should be dealt with?

Wanakamati wakifanya makosa ndani ya msitu wa kijiji wafanyweje?
Walenzi watapewa adhabu ipi endapo watafanya makosa katika kazi?

How much the fine or compensation should be? If the offender is a member of the forest committee or the village government, should the fine be doubled?
Other penalties? E.g. Could the offender be given some technical or communal work to compensate the offence? If the offender refuses, what should be done?
How to deal with members of the committee who abuse their position?
How forest guards are punished if they abuse their position?

- 9. TARATIBU ZA KUSHUGHULUKIA WAHALIFU**
(Matumizi yaliyopigwa marufuku na matumizi yanayohitaji kibali au leseni lakini mhalifu hakuwa na kibali au leseni, yaorodheshwe chini ya kifungu 9.1 au 9.2)

PROCEDURE OF PUNISHMENTS
(All forbidden uses and uses against the rules (e.g. use without a permit, when permit is required) should be listed under 9.1 and 9.2)

- 9.1 Makosa yatakayoshughulikiwa katika ngazi ya kijiji**
(Orodha ya makosa.)

Cases, that are dealt with at the village level
(List of cases.)

(Mwezeshaji ataandika sentensi ifuatayo na kujadiliwa na timu ya kuandaa mpango na sheria ndogo.)
Kama shitaka halikumalizika katika ngazi ya kijiji itapelekwa Mahakamani.

(The following sentence is written by the facilitator and discussed with the planning team.)
If the case can not be solved in the village level, it should be taken to the court.

9.2 Makosa yatakayoshughulikiwa katika ngazi ya Mahakama

(Orodha ya makosa.)

(Mwezeshaji ataandika sentensi ifuatayo na kujadiliwa na timu ya kuandaa mpango na sheria ndogo.)

Kwa matumizi yaliyopigwa marufuku yakitaka kupelekwa Mahakamani, serikali ya kijiji au kamati ya msitu ni lazima iombe ushauri au itoe taarifa kwa Mtendaji wa Kata na afisa misitu.

Aidha sheria ndogo inategemea fidia kurudishwa na Mahakama kijijini. Fidia hiyo itakayolipwa na mhalifu, itahusu gharama za kumkamata mhalifu na kumsafirisha hadi Mahakamani.

10. MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO

(Mwezeshaji ataandika sentensi ifuatayo na kujadiliwa na timu ya kuandaa mpango na sheria ndogo.)

Serikali ya kijiji, kupitia maazimio ya mkutano mkuu inaweza kubadili, kurekebisha au kusahihisha sheria ndogo hii ilikuongeza ufanisi endapo itaonekana haja ya kufanya hivyo. Marekebisho hayo ni lazima yaidhinishwe na Halmashauri ya Wilaya kabla ya kuanza kutumika.

11. TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

(Mwezeshaji ataandika sentensi ifuatayo na kujadiliwa na timu ya kuandaa mpango na sheria ndogo.)

Tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria ndogo hii ni baada ya kupitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya

SEHEMU YA TATU

12. SAHIHI

Saini za Mwenyekiti wa kijiji, Katibu/Afisa mtendaji wa kijiji, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya husika na Mkurugenzi mtendaji wa Wilaya.

Cases, that are dealt with in the court

(List of cases.)

(The following sentences are written by the facilitator and discussed with the planning team.)

If forbidden actions need to be taken to the court, the village government or the forest committee should take the issue to the Primary Court and consult and report to the Ward Executive Officer and the forest officer.

This by-law expects the court to return the compensation back to the village. This compensation, which is paid by the offender, should cover the costs occurred when taking the offender to the court.

AMENDMENTS

(The following sentences are written by the facilitator and discussed with the planning team.)

Village government, according to the decision of the village assembly, can change, adjust or correct this by-law for improvements, when need arises. All changes have to be approved by the District Council.

DATE OF COMMENCEMENT

(The following sentence is written by the facilitator and discussed with the planning team.)

Date of commencement is the date when the District Council has approved the by-law.

SECTION THREE

SIGNATURES

Signatures of village chairman, village secretary/executive officer, chairman of the district council and District Executive Officer.

Appendix 7. Example of JFM agreement

Appendix 7.1. In Swahili

**MAKUBALIANO YA UENDESHAJI WA PAMOJA WA ENEO LA MSITU LA KIJJI
KATIKA MSITU WA HIFADHI WA MTAI KATI YA IDARA YA MISITU NA NYUKI NA
KIJI CHATARAFI YA MARAMBA, WILAYA YA MUHEZA**

UTANGULIZI

Ofisi ya Hifadhi Misitu Tanga kwa niaba ya Idara ya Misitu na Nyuki, kwa mamlaka iliyopewa ya usimamizi na uendeshaji wa Msitu wa Hifadhi wa Mtai, na kijiji cha kwa pamoja wanakubaliana kuimarisha na kuboresha uendeshaji wa eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai kama linavyoonekana katika kiambatishi “A”, ili kuinua kiwango cha uhifadhi wa Misitu ya Usambara Mashariki. Sambamba na hayo, kutambua mahitaji ya wanakijiji ambayo hayapingani na uhifadhi endelevu wa misitu na bioanuai zake kama ilivyoainishwa katika mpango wa uendeshaji na uendelezaji msitu wa hifadhi wa Mtai (kiambatishi “B”), na sheria ndogo ya kutunza, kulinda na kuhifadhi msitu wa hifadhi wa Mtai (kiambatishi “C”) eneo la kijiji cha

Sehemu ya I: Jina la makubaliano

1. Jina la makubaliano haya litafahamika kama, makubaliano ya uendeshaji wa pamoja wa eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai, kati ya Idara ya Misitu na Nyuki na kijiji cha katika Tarafa ya Maramba, Wilaya ya Muheza.

Sehemu ya II: Madhumuni ya Makubaliano

2. Kuendesha kwa pamoja eneo la msitu la kijiji cha katika msitu wa hifadhi wa Mtai kwa njia ya uhifadhi shirikishi kwa kuzingatia mpango wa uendeshaji na sheria ndogo ya msitu, kama vilivyoandaliwa na kijiji kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa msitu wa hifadhi wa Mtai.
3. Kuelezea, kufafanua na kukubaliana juu ya haki za msingi na majukumu ya kijiji cha na yale ya Idara ya Misitu na Nyuki katika uendeshaji na utumiaji mazao ya misitu; na
4. Kuelezea na kukubaliana juu ya utaratibu wa kufikia na kutoa maamuzi juu ya masuala yanayohusu eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai.

Sehemu ya III: Uwakilishi wa wadau katika makubaliano.

5. Katika makubaliano haya, Idara ya Misitu na Nyuki itawakilishwa na Afisa Hifadhi Misitu Tanga, na Kijiji cha kitawakilishwa na mwenyekiti wa serikali ya kijiji.

Sehemu ya IV: Maelezo ya haki za kijiji na wanakijiji.

Katika makubaliano haya, kijiji cha kina haki zifuatazo katika eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai:

6. Kijiji kinatambulika kuwa ni miongoni mwa wadau wanaopakana na msitu wa hifadhi wa Mtai na kina haki ya kushiriki katika uendeshaji wa shughuli za msitu wa hifadhi wa Mtai;
7. Kijiji kina haki ya kuwasilisha hoja au pendekezo lolote kuhusu shughuli zinazohusiana na msitu wa hifadhi wa Mtai kwa Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki wakati wowote ule;
8. Wanakijiji wa kijiji cha wana haki zote za kunufaika kutokana na hifadhi ya msitu wa hifadhi wa Mtai kulingana na sera, sheria za misitu na taratibu za hifadhi zilizowekwa katika sheria ndogo za misitu za kijiji na mpango wa uendeshaji wa eneo la kijiji; na
9. Kijiji kitakuwa na haki ya kupata kiasi cha asilimia 40% ya mapato yatokanayo na mazao haramu ya msitu yaliyokamatwa na kutaifishwa na endapo kutakuwa na uvunaji halali toka eneo la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai.

Sehemu ya V: Majukumu na wajibu wa Serikali ya kijiji na wanakijiji

Serikali ya Kijiji cha inawajibika katika kutunza na kuendeleza eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai kama ifuatavyo:

10. Kuhakikisha kuwa mpango wa uendeshaji wa eneo la msitu la kijiji unapangwa na wanakijiji wenyewe na kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji kwa utekelezaji.
11. Kutunga na kutumia sheria ndogo ya msitu katika eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai.
12. Kuhakikisha kwamba taratibu zote za uendeshaji wa msitu wa hifadhi wa Mtai zinafahamika na kufuatwa na kila mwanakijiji kulingana na mpango wa uendeshaji na sheria ndogo ya msitu katika eneo la msitu la kijiji;
13. Kuanzisha kamati ya msitu ya kijiji ili kusimamia na kuratibu maswala ya hifadhi katika eneo la msitu la kijiji katika Msitu wa hifadhi wa Mtai; na
14. Kufanya marekebisho ya mpango wa uendeshaji wa msitu na sheria ndogo ya msitu pale inapobidi.
15. Kushirikiana na vijiji vinavyozunguka msitu wa hifadhi Mtai ili kuunda kamati ya kuratibu shughuli za uendeshaji wa msitu wa hifadhi

Sehemu ya VI: Haki za Idara ya Misitu na Nyuki.

16. Msitu wa Hifadhi wa Mtai utaendelea kuwa chini ya miliki ya Serikali Kuu chini ya Idara ya Misitu na Nyuki.
17. Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki – Tanzania, ana madaraka na maamuzi ya mwisho juu ya uendeshaji wa msitu wa hifadhi Mtai, endapo serikali ya kijiji ikishindwa kutekeleza au kusuluhisha mgogoro kwa ngazi iliyowekwa (kama ilivyoonyeshwa sehemu VIII) kwa kufuata

makubaliano haya.

18. Serikali itapata kiasi cha asilimia 60% ya mapato yatokanayo na mazao haramu ya msitu yaliyokamatwa na kutaifishwa na endapo kutakuwa na uvunaji halali toka eneo la uendeshaji la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai.

Sehemu ya VII: Majukumu na wajibu wa Idara ya Misitu na Nyuki

19. Idara ya Misitu na Nyuki, kwa kupitia Ofisi ya Hifadhi Misitu Tanga, itakuwa ni msimamizi mkuu wa Sera ya Taifa ya Misitu, Sheria ya Misitu na Programu ya Taifa ya Misitu, na itakuwa ni mwezeshaji mkuu wa mpango wa uendeshaji wa eneo la msitu eneo la kijiji.

Katika makubaliano haya, Idara ya Misitu na Nyuki itakuwa na majukumu yafuatayo:

20. Itashirikiana na serikali ya kijiji pamoja na kamati yake ya msitu katika kutekeleza shughuli zote za mpango wa uendeshaji eneo la msitu la kijiji katika msitu wa hifadhi wa Mtai;
21. Itajulisha na kuomba ushauri kutoka katika serikali ya kijiji kuhusu suala lolote linalohusu hifadhi hiyo ambalo kwa njia moja au nyingine litaathiri au kuhusisha kijiji hiki;
22. Kulipia gharama za kusafisha mipaka na kupanda miti ya mpaka wa nje na maeneo yaliyowazi ndani ya msitu katika eneo la msitu la kijiji, katika msitu wa hifadhi wa Mtai; na
23. Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu hifadhi ya misitu na uzuiaji wa mioto msituni, elimu ya miti mashambani na njia mbadala katika kupunguza kasi ya utegemezi wa mazao ya misitu na kuwezesha uanzishwaji wa kamati ya uratibu wa shughuli za msitu wa mtai.

Sehemu ya VIII: Mamlaka na taratibu za kutatua migogoro

24. Mgogoro wa aina yoyote wa uendeshaji ndani ya msitu wa hifadhi wa Mtai utasuluhishwa na Baraza la Usuluhishi la Kata.
25. Kama suluhu haikupatikana mgogoro huo utapelekwa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwa hatua zaidi.
26. Kama suluhu haikupatikana, Idara ya Misitu na Nyuki inaweza kusitisha haki za kijiji zitokanazo na hifadhi hii kwa muda, au moja kwa moja kwa taarifa ya miezi mitatu iwapo itabainika kuna ukiukwaji wa taratibu unaofanywa na kijiji, na kwamba uwezekano wa kurekebisha kasoro hizo haupo.
27. Serikali ya kijiji inaweza kusitisha utekelezaji wa mpango huu wa uendeshaji wa pamoja kwa taarifa ya miezi mitatu, endapo itabainika kwamba utekelezaji wa makubaliano haya umekiukwa, na kwamba hakuna suluhu inayoweza kupatikana.

Sehemu ya IX: Marekebisho ya makubaliano

28. Itakapobidi kufanya marekebisho yoyote ya makubaliano haya, pande zote mbili lazima

zitaarifiwe na zikubaliane kwanza kabla ya marekebisho hayo kufanyika.

29. Marekebisho yoyote yatakayofanywa kuhusiana na makubaliano haya ni lazima yaambatanishwe kama sehemu ya makubaliano haya.

Sehemu ya X: Kuanza kutumika na muda wa makubaliano

30. Makubaliano haya yataanza kutumika rasmi tarehe yatakaposainiwa na pande zote mbili.

31. Makubaliano haya yana nakala mbili zinazofanana, moja kwa kila upande.

Makubaliano haya yamesainiwa leo tarehe _____ mwezi wa _____ 2002

kati ya **Idara ya Misitu na Nyuki** na kijiji cha _____

1. KWA NIABA YA KIJJI:

Jina _____ Sahihi _____

Cheo _____

Mbele ya shahidi:

Jina _____ Sahihi _____

Cheo _____

2. KWA NIABA YA IDARA YA MISITU NA NYUKI TANZANIA BARA:

Jina _____ Sahihi _____

Cheo _____

Mbele ya shahidi:

Jina _____ Sahihi _____

Cheo _____

Nakala kwa taarifa:

Mkuu wa Wilaya, Muheza
Mkurugenzi Mtendaji (W), Muheza
Katibu Tarafa, Maramba
Afisa Mtendaji Kata, Maramba/ Mhinduro/ Kigongoi

Kiambatishi A

Ramani inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Hifadhi wa Mtai na vijiji vinavyozunguka msitu wa hifadhi wa Mtai na vilevile eneo la matumizi ya mazao ya misitu kwa ajili ya wanakijiji ndani ya msitu wa hifadhi wa Mtai.

Appendix 7.2. In English

MANAGEMENT AGREEMENT FOR THE VILLAGE FOREST MANAGEMENT AREA IN MTAI FOREST RESERVE BETWEEN THE FORESTRY AND BEEKEEPING DIVISION AND VILLAGE, OF MARAMBA DIVISION, MUHEZA DISTRICT

INTRODUCTION

On behalf of the Forestry and Beekeeping Division the Tanga Catchment Forest Office, which is having the mandate for the supervision and management of the Mtai forest reserve, and village unanimously agree to strengthen and improve the management of the village forest management area in Mtai forest reserve as shown in annex A, as well as to raise the level of conservation of the forests of the East Usambaras. At the same time the needs of the villagers are recognised in such a way that does not contradict sustainable forest management and conservation of its biodiversity as it is specified in the management plan for the village forest management area (annex B) and the by-law for managing, protecting and conserving Mtai forest reserve in the area of village (annex C).

Part I: Name of the agreement

1. The name of this agreement is joint management agreement for the village forest management area in Mtai forest reserve between the Forestry and Beekeeping Division and village, of Maramba Division, Muheza District.

Part II: Purpose of the agreement

2. To implement joint forest management in the village forest management area of village in Mtai forest reserve according to the management plan and by-law which have been made by the village with the objective to strengthen the conservation of Mtai forest reserve.
3. To define, clarify and mutually agree on the basic rights and responsibilities of village and those of the Forestry and Beekeeping Division concerning the management and utilization of forest products; and
4. To define and mutually agree on the procedures for proposing and making decisions on matters concerning the village forest management area in the Mtai forest reserve reserve.

Part III: Representation of stakeholders concerning the agreement

5. For this agreement, the Forestry and Beekeeping Division is represented by the Catchment Forest Officer Tanga and village is represented by the chairman of the village government.

Part IV: Defining the rights of the village and the villagers

According to this agreement village has the following rights in the village forest management area in Mtai forest reserve:

6. The village is recognised to be among the stakeholders bordering the Mtai forest reserve and it has the right to participate in the management activities of the Mtai forest reserve;
7. The village has the right to present any concern or recommendation concerning the activities of the Mtai forest reserve to the Director of Forestry and Beekeeping;
8. The villagers of village are entitled to benefit from this reserve according to the existing forest policy, forest act and the existing management procedures as defined in the management plan and by-law for the village forest management area; and
9. The village has the right to get 40% of the revenues from illegally harvested and confiscated products, and if there will be any legally harvested products in the village forest management area in Mtai forest reserve.

Part V: Duties and responsibilities of the village government and the villagers

The village government of village has the following responsibilities to conserve and develop the village forest management area in Mtai forest reserve:

10. To ensure that there is a forest management plan made by the villagers and approved in a village assembly and implemented;
11. To formulate and use by-law for forest conservation and development in the village forest management area in Mtai forest reserve;
12. To ensure that all forest management procedures of Mtai forest reserve according to the forest management plan and by-law for the village forest management area are known and followed by every villager;
13. To inaugurate a forest committee of the village in order to supervise and coordinate issues concerning protection in the village forest management area in Mtai forest reserve; and
14. To make adjustments in the forest management plan and by-law when needed.
15. To cooperate with villages bordering Mtai forest reserve in order to establish a coordinating committee for the management of the forest reserve.

Part VI: Rights of the Forestry and Beekeeping Division

16. Mtai forest reserve will continue to be under the authority of the Central Government under the Forestry and Beekeeping Division.

17. Director of Forestry and Beekeeping of Tanzania has the final responsibility and decision concerning Mtai forest reserve, if the village government fails to implement this agreement or if conflicts can not be solved as indicated in part VIII.
18. The Government will get 60% of the revenues from illegally harvested and confiscated products, and if there will be any legally harvested products in the village forest management area in Mtai forest reserve.

Part VII: Duties and responsibilities of the Forestry and Beekeeping Division

19. Forestry and Beekeeping Division represented by the Tanga Catchment Forest Office is the main supervisor for the forest policy, forest laws and the National Forest Programme, and the main facilitator of the management plan for the village forest management area.

According to this agreement the Forestry and Beekeeping Division has the following duties:

20. To cooperate with the village government and its forest committee in the implementation of all management activities of Mtai forest reserve in the village forest management area;
21. To inform and request advice from the village government concerning any matters related to this reserve which in one way or another will affect or involve this village;
22. To pay costs of border maintenance and border planting and enrichment planting of Mtai forest reserve in the village forest management area; and
23. To give technical advice on forest conservation and fire prevention, farm forestry and different measures in order to reduce the dependency on the forest products, and how to establish a coordinating committee for activities in Mtai forest.

Part VIII: Powers and procedures of resolving conflicts

24. Any type of conflict concerning the forest management of Mtai forest reserve is to be reconciled by the ward conciliation board.
25. If no solution is reached the matter must be brought forward to the District Executive Director's Office for further action.
26. If no solution is reached, Forestry and Beekeeping Division can suspend the rights of village temporarily or permanently after giving a notice three months in advance if there is clear evidence of infraction of regulations by the village and there are no possibilities to rectify.
27. Village government can suspend implementation of this joint management plan after giving a notice three months in advance in case it is evident that the implementation of this agreement has been infringed and it is not possible to get solution.

Part IX: Adjustments to the agreement

28. If any adjustments to this agreement are necessary both parties must first be informed and they should agree on these adjustments before they will be made.

29. Any adjustments concerning this agreement must be attached as an appendix to this agreement.

Part X: Date of commencement and duration of the agreement

30. This agreement will be effective from the day of signing by the both parties.

31. This agreement is made in duplicate, a copy for each party.

This agreement has been signed today on _____ (day) of _____ (month) 2002 between the Forestry and Beekeeping Division and _____ village.

1. ON BEHALF OF _____ VILLAGE

Name _____ Signature _____

Position _____

In the presence of:

Name _____ Signature _____

Position _____

2. ON BEHALF OF FORESTRY AND BEEKEEPING DIVISION OF TANZANIA

Name _____ Signature _____

Position _____

In the presence of:

Name _____ Signature _____

Position _____

Copy for information to:
 District Commissioner, Muheza,
 District Executive Director, Muheza
 Divisional Secretary, Maramba
 Ward Executive officer, Maramba/Mhinduro/Kigongoi

Annex A

Map showing the boundaries of the Mtai forest reserve and villages surrounding the Mtai forest reserve as well as the area for the villagers' use of forest products within the Mtai forest reserve

Appendix 8. Example of JFM management plan and by-law

Appendix 8.1. In Swahili

MPANGO WA UENDESHAJI NA UENDELEZAJI MSITU WA HIFADHI MTAI ENEO LA KIJIKI CHA MATEMBONI

1. UTANGULIZI

Msitu wa hifadhi Mtai ulihifadhiwa mwaka 1913, msitu huu ulihifadhiwa kutokana na umuhimu wake kwa Taifa. Msitu huu wenye hekta 3107 umeingia katika uhifadhi shirikishi kulingana na sera mpya ya misitu ya mwaka 1998. Msitu wa Hifadhi wa Mtai unazungukwa na vijiji vinane, ambavyo ni: Matemboni, Muzi-Kafishe, Maramba A, Maramba B, Hemsambia, Vuga, Kidundi na Kwekuyu.

Ili kutoa nafasi, kubwa kwa washikadau wote, kijiji cha Matemboni kilishiriki katika kubainisha mipaka ya ndani kati ya kijiji na kijiji, na nje ya msitu kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na utekelezaji wa mpango wa uendeshaji.

Aidha kijiji cha Matemboni kama ilivyo kwa vijiji vingine, kiliandaa mpango mahususi kwa lengo kuhifadhi, kuendeleza na kutumia mazao mbalimbali yaliyoruhusiwa na sheria ndogo waliyojitungia wenyewe.

Timu ya watu 17 (wanawake 5, wanaume 12) walichaguliwa na Serikali ya kijiji kwa lengo la kuandaa mpango. Wajumbe hao walipatikana kutokana na vigezo mbali mbali vilivyokubaliwa na wote. Uwakilishi wa mjumbe mmoja wa Serikali ya kijiji na wajumbe wanne (Mwenyekiti wa kitongoji, mwanaume mmoja, mwanamke mmoja na ulinzi/askari mmoja) kwa kila kitongoji kati ya vitongoji vinne vya kijiji hiki ambavyo ni Shule, Matumbili, Tewe na Majengo.

Rasimu ya mpango huu uliwasilishwa kwa Serikali ya kijiji ambayo nayo ina wajibu wa kuiwasilisha kwenye mkutano mkuu wa kijiji kwa uthibitisho kabla ya kuanza kutumika.

2. HISTORIA YA MSITU WA MTAI

Msitu wa hifadhi wa Mtai ulikuwa unalindwa kwa sheria iliyotungwa tangu enzi ya kikoloni, ambayo haikutoa nafasi kwa jamii kutumia/kufaidi mazao ya msitu huo. Pamoja na sheria hizo msitu huu uliendelea kupoteza ubora wake siku hadi siku kwa sababu uhalifu uliokuwa unafanywa na jamii haikuwa na nafasi ya kukemea uhalifu huo.

Kutokana na sera ya Misitu ya mwaka 1998, jamii imeanza kushirikishwa katika kulinda na kuendeleza msitu huu wenye mimea na wanyama adimu duniani.

Tathimini shirikishi ilitumika kwa washikadau wote wanaozunguka msitu huu, ambao walitoa mbinu sahihi za kuendeleza msitu huu na mbinu hizo kutumika katika kuandaa mpango huu.

3. ENEO, MIPAKA NA AINA ZA KANDA

3.1. Eneo na mipaka

Eneo la hifadhi la msitu chini ya kijiji cha Matemboni ni hekta 586.

Mipaka yake imegawanywa kwa kuzingatia mipaka ya kiutawala ya vijiji (kati ya kijiji na kijiji) na hali halisi ya msitu, lengo lake likiwa ni kurahisisha uangalizi, usimamizi na uendeshaji mzuri eneo husika.

Mipaka ya msitu wa Hifadhi wa Mtai kwa eneo la kijiji cha Matemboni

- Kwa upande wa Mashariki na Kaskazini eneo linapakana na eneo la msitu la kijiji cha Maramba 'B'
- Kwa upande wa Magharibi linapakana na kijiji cha Muzi–Kafishe
- Kwa upande wa Kusini limepakana na vitongoji vya Majengo na Tewe katika kijiji cha Matemboni.

Urefu wa mpaka wa msitu kwa nje ni kilomita 5.

3.2. Aina za kanda katika msitu wa Hifadhi wa Mtai – eneo la Matemboni

Eneo la msitu wa Mtai limegawanywa katika kanda nne kuu. Mgawanyo huo umefanywa kulingana na umuhimu au ubora wake katika msitu kwa kuzingatia matokeo ya utafiti uliokwishafanyika.

i. Kanda ya bioanuwai

Kanda hii inahusu sehemu iliyotengwa kwa ajili ya utunzaji wa mimea, wadudu, ndege na wanyama. Ili kutoa nafasi kwa uoto wa asili, itakuwa ni marufuku shughuli yeyote itakayodhuru viumbe hivi kufanyika katika kanda hii. Kanda hii imetengwa kwa kuzingatia ripoti ya utafiti ya bioanuai iliyofanyika mwaka 1997.

ii. Kanda za hifadhi ya maji

Kanda hizi zinahusu maeneo yenye vyanzo vya maji kama vile chemichemi, mito, vijito na ardhioevu. Hizi kanda kwa kiasi fulani ziliathirika kwa ukataji wa miti kwa matumizi mbalimbali. Hivyo ili kurekebisha hali hii na kurejesha ile hali ya awali, na pia kuhakikisha chemichemi na mito vinahifadhiwa na kuruhusu uoto wa asili, ni marufuku kufanya shughuli yoyote ile katika maeneo hayo. Maeneo haya ya mito na chemichemi katika ukanda wa matumizi yatahifadhiwa kulingana na sheria ya misitu, yaani eneo la mita 50 kwa pande zote mbili za mito, eneo la mita 30 kwa pande zote mbili za vijito na mita 20 kwa kila upande maeneo ya chemichemi na ardhioevu. Mito katika Hifadhi ya Mtai eneo la Matemboni ni Msaza, Tewe na Golan.

iii. Kanda ya matumizi

Kanda hii inahusu utunzaji wa misitu kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Katika kanda hii ndipo kuni, madawa n.k. yatachukuliwa lakini kwa utaratibu maalum utakaozingatia matumizi endelevu kama ilivyo bainishwa katika mpango huu na sheria ndogo (Sheria ndogo za kutunza, kulinda na kuhifadhi msitu wa hifadhi Mtai eneo la kijiji cha Matemboni kwa matumizi endelevu, za mwaka 2002) na utasimamiwa na kamati ya msitu ya kijiji. Ili kuongeza kipato cha wananchi, ufugaji wa nyuki utatiliwa mkazo katika kanda hii.

iv. Sehemu za tambiko

Sehemu hizi zitatengwa kwa ajili ya kufanyia matambiko tu. Watumiaji wanatahadharishwa kuwa makini katika kutumia moto wakati wa shughuli za matambiko. Eneo la Majengo na Tewe linatumika na Wakilindi. Vikundi vingine ambavyo havijabainishwa vitajadiliwa na kamati ya msitu kabla ya kuruhusiwa kufanya tambiko ndani ya msitu.

4. MALENGO YA KUHIFADHI MSITU WA MTAI – ENEO LA MATEMBONI

Tangu zamani msitu wa Mtai ulionekana kuwa ni wa muhimu kutokana na viumbe vilivyomo na vyanzo vingi vya maji vinavyoanzia humo. Kutokana na uharibifu uliokwisha fanyika, hali ya msitu huo imebadilika sana na inahatarisha maisha ya viumbe na chemichemi zilizosalia. Kwa hiyo basi, nia ni kurejesha ile hali yake ya awali. Ili kufanikisha azma ya hifadhi na matumizi endelevu, malengo yatakuwa kama ilivyo katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 1 Malengo ya Msitu wa hifadhi Mtai

LENGO KUU	MALENGO MAALUM	VIASHIRIO
Kuhifadhi rasilimali za msitu wa Mtai ili kuhifadhi ardhi na viumbe vilivyomo kwa matumizi endelevu kwa sasa na vizazi vijavyo.	Kutunza na kulinda msitu na viumbe wengine.	<ul style="list-style-type: none"> - Kupungua kwa matukio ya matumizi mabaya ya msitu. - Kupungua kwa matukio ya moto.
	Kushirikisha/kuelimisha wananchi Kijijini.	<ul style="list-style-type: none"> - Kuongezeka kwa matumizi mibadala ya mazao ya misitu. - Kuongezeka watu wanaokuza na kupanda miti.
	Kuimarisha vyanzo vya maji.	- Kudumu kwa maji katika vyanzo na vijito vya Tewe, Golan na Msaza.
	Kuzuia mmomonyoko wa udongo.	<ul style="list-style-type: none"> - Ongezeko la watu wanaolima kwa kutumia makingamaji. - Ongezeko la maeneo ya mashamba yaliyo na makingamaji.

5. TARATIBU ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA MSITU

Kwa mujibu wa mpango huu, msimamizi Mkuu wa mpango itakuwa ni Kamati ya Msitu wa Mtai. Kamati hii itachaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji kwa kuzingatia uwakilishi wa vitongoji vyote. Uchaguzi huu pia utazingatia jinsia. Kamati itawajibika kwa kutoa taarifa zao za kila mwezi kwa Serikali ya kijiji pamoja na ofisi ya hifadhi misitu. Kamati hii pia itakuwa na jukumu la kuchagua walinzi wa msitu na kupanga taratibu za doria. Muda wa kamati kuwa madarakani ni miaka mitatu na baada ya hapo kamati itavunjwa na kuundwa nyingine.

Sifa za mjumbe wa kamati ya msitu ni lazima awe mtu anayejituma, asiye na ubinafsi, anayejali maslahi ya Kijiji na Taifa kwa ujumla.

Katika kuchagua Kamati, vigezo vifuatavyo viliwekwa ili kuboresha utendaji wa kazi na majukumu. Kila kitongoji kihusishwe kwa kutoa wajumbe watano (pamoja na Mwenyekiti wake wa kitongoji, wengine watatu mmoja awe mwanaume na mwingine mwanamke na mjumbe wa tatu na wa nne ni askari). Jumla wajumbe wa Kamati ya msitu ni 20.

5.1. Madaraka na majukumu ya viongozi wa Kamati ya msitu

5.1.1. Mwenyekiti

Kamati itakuwa na Mwenyekiti ambaye ataongoza vikao vyote vya Kamati pamoja na kuhakikisha kuwa shughuli za msitu zinatekelezwa kama ilivyopangwa.

5.1.2. Katibu

Kazi ya Katibu itakuwa ni kuratibu shughuli zote za msitu chini ya Mwenyekiti wa msitu. Atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa masuala yanayohusu msitu. Shughuli nyingine zitakuwa ni kuandaa vikao vinavyohusu msitu, pamoja na kutunza kumbukumbu zote zinazohusu msitu wa Mtai eneo la kijiji cha Matemboni.

5.1.3. Mtunza fedha

Kamati itatumia Mtunza fedha wa Kijiji katika shughuli zake. Atasimamia kupokea mapato na matumizi ya fedha za msitu na kutunza kumbukumbu zote za fedha. Atawajibika kutoa vitabu vya fedha kwa wakaguzi wa ndani na wa nje vitakapohitajika. Aidha anatakiwa kutoa kila mwezi taarifa za mapato na matumizi ya fedha kwa mwenyekiti wa kamati.

5.1.4. Walinzi wa msitu

Kutakuwepo na walinzi wa msitu ambao watashughulikia masuala ya doria, usimamiaji na utekelezaji wa sheria ndogo za msitu. Walinzi hawa watachaguliwa kama ilivyoainishwa hapo awali. Mbali na kuendesha shughuli za doria, walinzi watawajibika kupeleka taarifa zao za utendaji kwa Mwenyekiti/Katibu wa Kamati ya Msitu, ambaye naye atazifanyia kazi au kuzipeleka kwa Serikali ya Kijiji.

5.2. Vikao vya Kamati

Kamati itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi miwili, isipokuwa endapo kuna dharura kikao kinaweza kikafanyika wakati wowote kulingana na dharura yenyewe. Endapo mjumbe atakosa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila taarifa atakuwa amejivua ujumbe wa Kamati na nafasi yake itajazwa kwa kuzingatia taratibu za kawaida za uchaguzi katika kijiji.

5.3. Wajibu wa wadau

5.3.1. Wanakijiji

- Kulinda msitu
- Kuzima moto
- Kutekeleza shughuli za uendeshaji na uendelezaji wa msitu

5.3.2. Serikali ya kijiji

- Kusimamia mapato na matumizi ya msitu
- Kuitisha mikutano
- Kuelimisha wanakijiji
- Kutunga na kusimamia sheria ndogo

5.3.3. Halmashauri ya wilaya

- Kupitisha sheria ndogo za vijiji
- Kuboresha huduma za jamii vijijini

5.3.4. Serikali kuu

- Kulipia gharama za uimarishaji wa mipaka (kama upandaji wa miti na usafishaji wa mipaka)
- Kulipia gharama za ukarabati wa msitu (kama upandaji wa miti katika maeneo yaliyowazi ndani ya msitu)
- Kutoa utalam wa kuelimisha wanakijiji kwa ajili ya kuendesha msitu (kama vile uandaaji wa vitalu na kupanda miti)

6. SHUGHULI ZA UENDESHAJI

Ili kufikia malengo ya kuhifadhi msitu wa Mtai, kutakuwa na shughuli zitakazokuwa zikifanywa na wananchi ili kuendeleza na kulinda msitu huu kwa faida ya wote. Shughuli zitakazofanyika ni kama zifuatazo:

Jedwali Na. 2 Shughuli za Uendeshaji

NA	SHUGHULI	LENGO	WAHUSIKA	MUDA/KIPINDI
1	Ulinzi/Doria	Kuzuia uhalifu	Wananchi, walinzi	Wakati wote
2	Kulimia mipaka	Kuzuia moto	Wananchi, Idara ya misitu	Mara mbili kwa mwaka Januari - Februari, Agosti - Septemba
3	Kupanda miti sehemu zilizo athirika	Kurudisha uoto wa asili kwa sehemu zilizoathirika	Kamati ya msitu wataalamu, na wanakijiji.	Mara mbili kwa mwaka Aprili - Mei, Oktoba - Novemba
4	Kuweka vitalu	Kupata miche	Wanakijiji, Idara ya misitu	Juni, Julai na Agosti
5	Kutunza vyanzo vya maji na chemichemi	Kuzuia ukame na uhaba wa maji	Kamati ya msitu wanakijiji na serikali ya kijiji	Wakati wote
6	Kutambua maeneo ya tambiko	Kulinda mila na desturi/ utamaduni	Wanakijiji na kamati ya msitu.	Wakati ulioruhusiwa

NA	SHUGHULI	LENGO	WAHUSIKA	MUDA/KIPINDI
7	Kuelimisha na kuhamasisha wanakijiji	Kupunguza uhalifu. Kuongeza elimu ya miti na viumbe adimu	Kamati ya msitu wataalamu Serikali ya kijiji	Wakati unaojulikana
8	Kutambua eneo la kijiji	Kudhibiti eneo husika	Wanakijiji	Wakati wote
9	Kufungua akaunti na kukusanya mapato ya kamati	Kupata fedha za kuendeshea shughuli za msitu	Kamati ya msitu	Wakati wote
10	Kujenga ofisi ya msitu	Kupata ofisi ya kufanyia kazi	Kamati ya msitu, wananchi, Serikali ya kijiji na wataalam	Wakati utakaopangwa

7. UKAGUZI NA ULINZI WA MSITU WA MTAI

- i. Itakuwa ni jukumu la kamati ya msitu kuhakikisha inateua walinzi wa kufanya doria katika msitu wa Mtai eneo la kijiji ili kudhibiti uharibifu wa msitu. Ulinzi huu utafanywa kwa zamu kadri itakavyopangwa.
- ii. Mwenyekiti wa kitongoji anawajibu wa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya msitu katika kitongoji chake yanatunzwa kama ilivyo katika sheria ndogo ya msitu.
- iii. Itakuwa ni jukumu la kamati ya msitu kuhakikisha kuwa vitongoji vinadhiti uharibifu wa msitu. Kamati hii pia inayo mamlaka ya kumkamata mhalifu na kumfikisha katika baraza la kijiji.
- iv. Kila mwanakijiji wa kijiji cha Matemboni atawajibika kuhakikisha kuwa uharibifu haufanyiki katika msitu wa Mtai kwa kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Kitongoji au Katibu wa kijiji cha Matemboni au katika kamati ya msitu.
- v. Ishara ya gunda itatumika kuwajulisha wanakijiji wa Matemboni kuhusu tukio la moto msituni na ni jukumu la kila mwanakijiji kushiriki katika kuzima moto.
- vi. Kiongozi yeyote wa serikali ya kijiji cha Matemboni anayo mamlaka ya kumkamata mtu yeyote anayefanya kosa kinyume cha Sheria ya kijiji na kumfikisha katika baraza la kijiji kwa hatua za kisheria.

8. MASHARTI NA TARATIBU ZA KUHFADHI MSITU WA MTAI - ENEO LA MATEMBONI

Masharti na taratibu za kuhifadhi msitu wa Mtai, ikiwa ni pamoja na matumizi yake, yatakuwa kama yalivyofafanuliwa katika mpango huu, pamoja na sheria ndogo ya msitu.

8.1. Matumizi yaliyopigwa marufuku katika msitu wa hifadhi

Mtu yeyote atakayefanya matendo yafuatayo katika msitu wa hifadhi Mtai atakuwa amevunja sheria ndogo ya msitu:

- i. Kuchoma mkaa na kukata kuni mbichi.
- ii. Kuharibu sehemu za kufanyia tambiko na vyanzo vya maji.

- iii. Kulima ndani ya msitu.
- iv. Kurina asali mwitu.
- v. Kuwinda wanyama, kuvua samaki.
- vi. Kuchimba madini na kuzoa mchanga.
- vii. Kufyeka msitu kwa madhumuni ya makazi au shamba.
- viii. Kuchunga mifugo, kukata nyasi kwa ajili ya mifugo na kuezeka nyumba.
- ix. Kuwasha au kuchoma moto msitu
- x. Kufungua njia/barabara mpya ndani ya msitu.
- xi. Kupasua mbao
- xii. Kukata nguzo, mapau, fito na kamba za kuchubua miti
- xiii. Kukusanya mazao ya msitu kwa biashara

8.2. Matumizi yanayohitaji kibali

Matumizi yafuatayo yatafanyika pale tu kibali imetolewa kulingana na mpango wa msitu wa hifadhi Mtai:

- i. Kukata kamba za kutambaa kwa ajili ya ujenzi (kibali toka kamati ya msitu)
- ii. Kuokota mawe (kibali toka Kamati ya msitu na Idara ya Misitu)
- iii. Kuchimba mifereji ya maji/bomba (kibali toka Kamati ya msitu na Idara ya Misitu)
- iv. Kufuga nyuki (kibali toka Kamati ya msitu)
- v. Kufyeka njia za miguu za asili (kibali toka Kamati ya msitu)
- vi. Kuingiza wageni kwa ajili ya mafunzo/utafiti (kibali toka Kamati ya msitu)

8.3. Matumizi huru ya mazao ya misitu kwa wakazi wa Matemboni

Mwananchi/wananchi wa kijiji cha Matemboni anaruhusiwa/wanaruhusiwa kufanya vitendo hivi vifuatavyo:

- i. Kuchota maji kwenye vyanzo vya maji vilivyoruhusiwa
- ii. Kuokota kuni kavu kwa matumizi ya nyumbani kwa siku iliyoruhusiwa tu (mara mbili kwa wiki)
- iii. Kuchuma mboga za majani na uyoga kwa matumizi ya nyumbani
- iv. Kuchimba/kuchuma dawa kwa matumizi ya nyumbani
- v. Kufanya tambiko
- vi. Kutumia njia za asili za miguu

9. NAMNA YA KUSHUGHULIKIA MAKOSA YATAKAYOFANYIKA NDANI YA MSITU NA NDANI YA ENEO LA MATEMBONI

Kwa kulingana na sheria ndogo ya msitu, mhalifu yeyote atakayekamatwa atafikishwa katika Kamati ya msitu, ambayo italipeleka suala lake katika Baraza la kijiji na kutafutiwa ufumbuzi kulingana na sheria ndogo ya msitu. Ikishindikana kupata utatuzi, basi suala lake lipelekwe Mahakamani, likisimamiwa na Kamati kwa niaba ya kijiji na wataalam wa msitu.

10. UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

Kumbukumbu zote muhimu zinazohusu msitu wa Mtai eneo la Matemboni zitatunzwa na watendaji wafuatao:

- Taarifa zote za kazi mtunzaji ni Katibu wa Kamati ya msitu.
- Kitabu cha doria kitatunzwa na kiongozi wa ulinzi.
- Kitabu cha vibali mtunzaji ni Katibu wa Kamati ya msitu.
- Kumbukumbu zote za uhalifu watunzaji ni Katibu wa Kamati ya msitu na Katibu wa Baraza la kijiji.
- Stakabadhi ya malipo mtunzaji ni Mtunza fedha wa kijiji.
- Kitabu cha mapato na matumizi mtunzaji ni Katibu wa Kamati ya msitu.

11. UTUNZAJI WA MAPATO NA MATUMIZI YA MSITU

11.1. Vyanzo vya mapato

- i. Faini mbalimbali
- ii. Ada za wageni mbalimbali
- iii. Vibali/Ushuru mbalimbali
- iv. Mnada wa mazao ya msitu na mali ya mhalifu itakayotafishwa
- v. Wahisani/mikopo mbalimbali
- vi. Malipo kutokana na uimarishaji wa mipaka na ukarabati wa msitu .

11.2. Viwango vya ada kwa wageni

Ada za kuingiza wageni kwa Watanzania ni Tsh. 500/= kwa kichwa na Dola tatu (3) za Marekani kwa wasio Watanzania kwa kichwa au kiasi sawa na hicho kwa fedha za Tanzania. Viwango hivi vinaweza kufanyiwa marekebisho wakati wowote Serikali ya kijiji itakavyoona inafaa.

11.3. Akaunti ya hifadhi ya msitu

- Kamati ya msitu itafungua akaunti ya hifadhi ya msitu Matemboni
- Akaunti hii itatumika kuhifadhi mapato yote ya fedha za msitu
- Mtunza fedha atawajibika na utunzaji wa akaunti ya hifadhi ya msitu
- Ni Mwenyekiti wa kamati ya msitu, Katibu wa kamati ya msitu, Mtunza fedha wa Kijiji na Mjumbe mmoja (mwanamke aliyechaguliwa na kamati kwa ajili hiyo) watahusika katika kuweka na kuchukuliwa fedha kutoka kwenye akaunti ya hifadhi ya msitu

11.4. Taratibu za utunzaji fedha

- Kutakuwa na vitabu vya kupokelea na kutolea fedha (stakabadhi ya fedha na hati ya malipo).
- Mtunza fedha atakuwa mtunza fedha wa kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa mahesabu atakuwa Katibu wa kamati ya msitu wa kijiji.
- Ukaguzi wa nje utafanywa na Afisa Ushirika wa Tarafa au Wilaya.
- Ukaguzi huo utafanyika kila baada ya miezi mitatu.
- Serikali ya Kijiji ndio itatoa idhini ya matumizi ya mapato

11.5. Matumizi ya fedha za msitu

- Motisha kwa wajumbe wa kamati ya msitu.
- Posho kwa walinzi na wajumbe wakipeleka wahalifu polisi na kusimamia kesi Mahakamani.

- Gharama za utunzaji wa vitalu vya miti kijijini.
- Kununua vifaa vya ofisi (vitendea kazi).
- Wajumbe kwenda na kurudi kwenye vikao vya kuendeleza msitu au ziara za mafunzo.
- Kugharamia shughuli za maendeleo ya kijiji (kama ujenzi wa ofisi ya kijiji)
- Asilimia 50 ya malipo kutokana na uimarishaji wa mipaka au ukarabati wa msitu yatalipwa kwa wananchi watakaoshiriki katika kazi hizo, na asilimia 50 nyingine itakuwa ni mchango wao kwenye akaunti ya hifadhi ya msitu. Asilimia hizi zinaweza kufanyiwa marekebisho na mkutano mkuu wa kijiji endapo itaonekana haja ya kufanya hivyo.

11.6. Utaratibu wa kuuza mazao ya msitu yaliyokamatwa

Mali mbalimbali zitakazokamatwa na walenzi ndani ya msitu kama mbao, misumeno, mapanga n.k. zitahifadhiwa katika ofisi ya kijiji. Mali hizo au vifaa hivyo pindi vikitaka kuuzwa mnada wa hadhara utumike kupunguza urasimu. Mnada huu utaendeshwa na Kamati ya msitu na Idara ya Misitu. Serikali ya kijiji ipewe 40% na Serikali kuu 60% .

12. UFUATILIAJI NA TATHMINI YA SHUGHULI ZA UENDESHAJI MSITU WA MTAI

Mbali na kuwa na Kamati ya Msitu na walenzi ambao watakuwa wanatekeleza shughuli za kila siku, kutakuwepo na suala la ufuatiliaji na utoaji wa taarifa na kufanya tathmini kwa kuangalia malengo na viashirio ili kupima mafanikio yaliyofikiwa.

Kazi hii itafanywa na wahusika mbalimbali kama vifuatavyo:

Jedwali Na. 3 Ufuatiliaji na tathmini ya shughuli

MADA	NANI	NINI	MUDA
Ufuatiliaji wa shughuli za uendeshaji.	Kamati ya maliasili ya kijiji.	Shughuli zote kama zinatekelezwa kwa kufuata mpango.	Muda wote kufuatana na mahitaji.
Tathmini ya shughuli za uendeshaji, majukumu, malengo na mafanikio.	Wataalam wa misitu na viongozi ngazi ya Kata/Tarafa.	Tathmini ya shughuli zote za msitu wa Mtai eneo la Matemboni zinazoendeshwa na Kamati na kutoa taarifa.	Baada ya kipindi cha majaribio na kila baada ya miaka mitatu ya uendeshaji.

Kipindi cha majaribio itakuwa miaka miwili tangu kuanza kutumika mpango huu.

KIJIJI CHA MATEMBONI

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (SERIKALI ZA VIJIJI 1982)

SHERIA NA. 7 YA 1982

SHERIA NDOGO

ZILIZOUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 120 (1) NA (163)

SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Sheria ndogo hii imetungwa kwa lengo la kulinda, kuendeleza na kuweka matumizi endelevu ya rasilimali za msitu wa hifadhi Mtai eneo la kijiji cha Matemboni kilichoko Kata ya Mhinduro, Tarafa ya Maramba, Wilaya ya Muheza na Mkoa wa Tanga.

Sheria ndogo hii imetungwa sambamba na mpango wa uendeshaji wa msitu huo. Aidha imezingatia lengo la kuhifadhi, hali halisi ya msitu na mazingira yake.

2. JINA LA SHERIA NDOGO

Sheria ndogo hii iitwe sheria ndogo ya mwaka 2002 za kutunza, kulinda na kuhifadhi msitu wa hifadhi Mtai eneo la kijiji cha Matemboni kwa matumizi endelevu.

3. TAFSIRI YA MANENO

- ◆ **Afisa misitu** - Maana yake ni mtaalam wa Idara ya misitu na Nyuki atakayesimamia na kutoa ushauri kwa shughuli zinazohusu hifadhi ya misitu katika kijiji cha Matemboni.
- ◆ **Bioanuwai** - Maana yake ni uwiano kati ya mimea na viumbe wengine katika eneo moja.
- ◆ **Eneo la msitu la kijiji cha Matemboni** - Maana yake ni sehemu ya msitu wa hifadhi wa Mtai lililoko katika kijiji cha Matemboni chini ya usimamizi shirikishi wa kamati ya msitu ya kijiji cha Matemboni na Idara ya Misitu na Nyuki.
- ◆ **Kamati ya maliasili** - Maana yake ni kamati iliyochaguliwa na serikali ya kijiji cha Matemboni ili kusimamia na kuratibu maswala yote ya hifadhi ya mazingira katika ngazi ya vijiji husika.
- ◆ **Kamati ya msitu** - Maana yake ni wajumbe waliochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji cha Matemboni ili kusimamia shughuli zote za msitu wa hifadhi Mtai eneo la kijiji cha Matemboni kwa niaba ya wanakijiji.
- ◆ **Katibu wa kamati ya msitu** - Maana yake ni Katibu aliyechaguliwa na wanakamati kuratibu shughuli za kila siku za msitu wa Mtai eneo la kijiji na kutunza kumbukumbu za msitu.
- ◆ **Katibu wa kijiji** - Maana yake ni mtu aliye chaguliwa kufanya kazi za ukatibu wa serikali ya kijiji cha Matemboni.
- ◆ **Kibali** - Maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na mamlaka husika kufanya tendo/jambo fulani ndani na nje ya msitu wa hifadhi.

- ◆ **Kitongoji** - Maana yake ni sehemu ya kijiji cha Matemboni kama inavyofahamika na kijiji cha Matemboni ndani ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.
- ◆ **Leseni** - Maana yake ni kibali cha maandishi kinachoambata na stakabadhi ya malipo, kinachoruhusu uvunaji au utumiaji wa mazao ya misitu kwa masharti yaliyowekwa.
- ◆ **Mazao ya misitu** - Ni mazao yote yaliyo timbao na yasiyo timbao, ikiwa ni pamoja na udongo, mchanga, kokoto, mawe, asali, nta, mimea, wanyama, ndege, wadudu na vyote vilivyomo juu ya uso wa ardhi.
- ◆ **Mifugo** - Maana yake ni wanyama wote wafugwao ambao huishi kwa kula miti, majani na nyasi, hii ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, nguruwe na kadhalika.
- ◆ **Mlinzi/walinzi wa msitu** - Maana yake ni mtu au watu waliochaguliwa na kamati ya msitu kufanya kazi ya doria au ulinzi katika msitu wa Mtai eneo la kijiji.
- ◆ **Mpango wa uendeshaji** - Maana yake ni mpango ulioandaliwa na wanakijiji cha Matemboni kwa minajili ya kuendesha shughuli za kuendeleza na kusimamia Msitu wa Mtai eneo la kijiji cha Matemboni.
- ◆ **Msitu wa hifadhi wa Mtai** - Maana yake ni msitu wa hifadhi wa serikali kuu katika Tarafa ya Maramba uliohifadhiwa kwa mujibu wa sheria za misitu.
- ◆ **Mwenyekiti wa kamati ya msitu** - Maana yake ni Mwenyekiti aliyechaguliwa na wanakamati kuongoza kamati ya msitu katika kusimamia shughuli zote za msitu wa Mtai eneo la kijiji.
- ◆ **Mwenyekiti wa kijiji** - Maana yake ni mwenyekiti wa serikali ya kijiji cha Matemboni kwa mujibu wa sheria za kijiji.
- ◆ **Mwenyekiti wa kitongoji** - Maana yake ni mtu yeyote aliyechaguliwa kuchukua madaraka ya uenyekiti katika ngazi ya kitongoji katika kijiji cha Matemboni kwa mujibu wa taratibu za kijiji.
- ◆ **Serikali ya kijiji** - Maana yake ni serikali ya kijiji cha Matemboni kwa mujibu wa sheria za kijiji.

4. ENEO NA MIPAKA YA MSITU WA HIFADHI WA MTAI KWA ENEO LA KIJJI CHA MATEMBONI

Eneo la msitu wa hifadhi chini ya kijiji cha Matemboni ni hekta 586.

Mipaka ya msitu wa hifadhi wa Mtai kwa eneo la kijiji cha Matemboni:

- Kwa upande wa Mashariki na Kaskazini eneo linapakana na eneo la msitu la kijiji cha Maramba 'B'
- Kwa upande wa Magharibi linapakana na eneo la msitu wa kijiji cha Muzi-Kafishe
- Kwa upande wa Kusini limepakana na vitongoji vya Majengo na Tewe katika kijiji cha Matemboni.

5. MWANGALIZI MKUU WA MSITU KATIKA ENEO LA KIJJI CHA MATEMBONI

Mwangalizi mkuu wa msitu katika eneo la kijiji cha Matemboni ni kamati ya msitu ambayo ndio itapanga walinzi wa msitu watakao toka katika vitongoji. Kamati hiyo itapeleka ripoti zake katika Serikali ya kijiji.

Kamati ya msitu itachaguliwa na mkutano mkuu na itadumu kwa kipindi cha miaka mitatu.

SEHEMU YA PILI

6. MATUMIZI YA MAZAO YA MSITU

6.1. Matumizi yaliyopigwa marufuku katika msitu wa hifadhi

Mtu yeyote atakayefanya matendo yafuatayo katika msitu wa hifadhi Mtai atakuwa amevunja sheria ndogo ya msitu:

- i. Kuchoma mkaa na kukata kuni mbichi.
- ii. Kuharibu sehemu za kufanyia tambiko na vyanzo vya maji.
- iii. Kulima ndani ya msitu.
- iv. Kurina asali mwitu
- v. Kuwinda wanyama, kuvua samaki.
- vi. Kuchimba madini na kuzoa mchanga.
- vii. Kufyeka msitu kwa madhumuni ya makazi au shamba.
- viii. Kuchunga mifugo, kukata nyasi kwa ajili ya mifugo na kuezeka nyumba.
- ix. Kuwasha au kuchoma moto msitu.
- x. Kufungua njia/barabara mpya ndani ya msitu.
- xi. Kupasua mbao
- xii. Kukata nguzo, mapau, fito na kamba za kuchubua miti
- xiii. Kukusanya mazao ya msitu kwa biashara.

6.2. Matumizi yanayohitaji kibali

Matumizi yafuatayo yatafanyika pale tu kibali/leseni imetolewa kulingana na mpango wa msitu wa hifadhi Mtai:

- i. Kukata kamba za kutambaa kwa ajili ya ujenzi (kibali toka kamati ya msitu)
- ii. Kuokota mawe (kibali toka Kamati ya msitu na Idara ya Misitu)
- iii. Kuchimba mifereji ya maji/bomba (kibali toka Kamati ya msitu na Idara ya Misitu)
- iv. Kufuga nyuki (kibali toka Kamati ya msitu)
- v. Kufyeka njia za miguu za asili (kibali toka Kamati ya msitu)
- vi. Kuingiza wageni kwa ajili ya mafunzo/utafiti (kibali toka Kamati ya msitu)

6.3 Matumizi huru ya mazao ya misitu kwa wakazi wa Matemboni

Mwananchi/wananchi wa kijiji cha Matemboni anaruhusiwa/wanaruhusiwa kufanya vitendo hivi vifuatavyo:

- i. Kuchota maji kwenye vyanzo vya maji vilivyoruhusiwa
- ii. Kuokota kuni kavu kwa matumizi ya nyumbani kwa siku iliyoruhusiwa tu (mara mbili kwa wiki)
- iii. Kuchuma mboga za majani na uyoga kwa matumizi ya nyumbani
- iv. Kuchimba/kuchuma dawa kwa matumizi ya nyumbani
- v. Kufanya tambiko
- vi. Kutumia njia za asili za miguu

7. UKAGUZI NA ULINZI WA MSITU WA MTAI

- i. Itakuwa ni jukumu la kamati ya msitu kuhakikisha inateua walenzi wa kufanya doria katika msitu wa Mtai eneo la kijiji ili kudhibiti uharibifu wa msitu. Ulinzi huu utafanywa kwa zamu kadri itakavyopangwa.
- ii. Mwenyekiti wa kitongoji anawajibu wa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya msitu katika kitongoji chake yanatunzwa kama ilivyo katika sheria ndogo ya msitu.
